

SPACE SCOOP

Bringing news from across the Universe to kids all around the world



Timu A ni ya Kimataifa



Katika kila pande ya Dunia kuna wanaanga wanashughulika. Baadhi yao wanafanya kazi katika vituo vya kuchungaza anga vya kiastronomia, wengine wanafanya kazi katika vyuo vikuu au katika taasisi za utafiti.

Picha hii inaonyesha kituo kipyta cha kuchunguza anga kilichopo Uholanzi, kiitwacho LOFAR. Awali Kilikuwa kinafanya kazi ya kuchunguza vitu ambavyo bado havijavumbuliwa katika ulimwengu. Mamia ya wanasayansi wanaanga kutoka katika pande mbali mbali za Dunia wamekuwa wakikitumia kituo cha LOFAR kwa shughuli zao za utafiti.

Wanaanga hawa hufanya kazi kwa pamoja kutoka sehemu mbali mbali Duniani na hutumia zana za mtandao (online tools), kama barua pepe na simu za video. Pia hupanga kutembeleana katika ofisi zao na kukutana katika mikutano ya kimataifa ya astronomia. Pindi wanapofanya ugunduzi, wanaanga huchapisha uvumbuzi wao kama timu moja.

Kwa mfano, chapisho la karibuni kutoka LOFAR lilihusisha timu kubwa ya wanaanga 84 kutoka katika vyuo na vituo vya utafiti 26 vilivyopo katika nchi 9! Walitumia LOFAR kuchunguza kundi la galaxi lililoitwa galaxy cluster (mkusanyiko wa galaxi). Timu hii iliona kuwa mawimbi redio yanayotoka katika galaxi cluster yalikuwa makali kuliko walivytarajia. Walifiki ni kwa sababu yalikuwa yakinkinzana na mkusanyiko mdogo wa galaxi.

Wanaanga hawa wamesambaza ugunduzi huo mpya na kwa wanaanga wengine wote Duniani. Wanaanga hufanya kazi kwa pamoja na hubadilisha mawazo wakutanapo katika mikutano ya kimataifa, ambayo watu wengi hiifa Jamii na wanaanga "Astronomy Community". Kitu kinachofanya ionekane kama kuna kijiji fulani ambamo wanaanga huishi pamoja.

COOL FACT

Wanaanga wana fikra kuwa LOFAR itafanikiwa kuvumbua zaidi ya vitu 100,000,000 ambavyo havijavumbuliwa bado na viro mbali kabisa katika ulimwengu.



ASTRON

More information about EU-UNAWE
Space Scoop: www.eu-unawe.org/kids/